# GATUZI NDOGO LA KIGUMO 2016
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI 102/2

**Ufahamu**.

(a) Alisingiziwa kumuua mtu.

(b) (i) Wafungwa hudhulumiwa
(ii) Kuna uvundo
(iii) Hakuna hewa safi
(iv) Watu hawaogi
(v) Kuna giza na joto
(vi) Kuna rundo la wafungwa (msongamano)

*(zozote 1 x 4 = al 4)*

(c) Wasomi ambao wamepewa majukumu ya kuwakilisha maslahi ya raia ndio wanaowadhulumu.

*(1 x 2 = al 2)*

(d) Hakuamini alikuwa kweli kaachiliwa huru.
Alihofia kuamuriwa asimame.
Alihofia kushukiwa bunduki.

*(1 x 3 = al 3)*

(e)(i) Mwema
(ii) Mwadilifu
(iii) Mkweli

*Zozote mbili (1 x 2 = al 2)*

(f)(i) Kitu kilichowazi.

*(1 x 1 = al 1)*

(ii) Hamu kubwa ya kufurahia kitu. *(1 x 1 = al 1)*

**Ufupisho** (al 15)

(a) *Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi?* (*al 7, 1 utiririko*)

- Tunapinga na kulaani visa vya ugaidi.
- Ugaidi ni kitendo cha kinyama kinachotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu.
- Ugaidi hauna uhusiano na dini yoyote.
- Polisi wanazembea katika kuzuia matendo ya kigaidi.
- Polisi wabuni njia mbadala ya kukabiliana na ugaidi badala ya kunasa raia wasio na hatia.
- Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama.
- Magaidi watalipia matendo yao.
- Wakenya wana haki ya kulindwa kikatiba.

*(hoja zozote7 x 1 = 7, al 1 ya utiririko)*

(b) *Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho*. (*al 6, 1 utiriko*)

- Raia wasio na hatia hunaswa.
- Hurundikwa kwenye seli na kuachiliwa huru kama wameteseka.
- Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu.
- Hii ni hila ya polisi kujionyesha kuwa wanafanya kazi.
- Magaidi huendesha shughuli zao.
- Polisi wanapaswa kubuni njia zitakazowapa mwelekeo mwafaka kuhusu wahalifu.
- Ushirikianao wa usalama kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**Matumizi ya lugha.**

(a)(i) f - mdomo meno.
(ii) dh - meno

*(1 x 2 = 2 mks)*

(b) (i) Kutenga sehemu ambayo haipaswi kuwa katika sentensi.
(ii) Kufungia neno lenye maana sawa na lililotajwa.
(iii) Kufungia tarakimu / herufi.
(iv) Katika maandishi ya kitamthilia kufungia maelezo ya nathari.

*(zozote 2 x 1 = 2)*

(c) <u>Si</u>tamsalimia mtoto <u>as</u>iye nadhifu.

*(2 x 1 = 2)*

(d) Tajiri ali<u>ye</u>sifiwa ame<u>ba</u>rikiwa.

*(2 x 1 = 2)*

(e) ✓✓“Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa maskini.✓✓”Mwalimu alitwambia.✓

($^1/_2$ *x 6 = 3*)

(f) (i) Fisha
(ii) Jiana

*(2 x 1)*

(g) Tulipo<u>vi</u>ona✓ <u>vi</u>likuwa✓ <u>vi</u>kichezea✓ <u>vi</u>jisu✓ vikali.

*(4 x $^1/_2$ = 2)*

(h) <u>M</u>✓wazima, <u>a</u>✓takurudishia.

*(1 x 2 = 2)*

(i)

| S✓ | | | |
|---|---|---|---|
| KN✓ | KT✓ | | |
| N ✓ | T ✓ | $KN_2$✓ | |
| | | N✓ | V✓ |
| Soka | ni | mchezo | maarufu |

*($8 \times {}^1/_2 = 4$)*

(j) Mwashi alimjengea shangazi nyumba kwa matafali.
kitondo kipozi Ala

*Mwalimu akadirie sentensi yoyote sahihi*

*(3 x 1)*

(k) Anapenda kula - Kirai kitenzi.
Mara nyingi - Kirai kielezi.

*(2 x 1 = 2)*

(l) Ingawa tulifika mapema - kishazi tegemezi.
Hatukumkuta - kishazi huru.

*(2 x 1 = 2)*

(m)(i) Karatasi - I - ZI
(ii) Kipepeo - A - wa

*(2 x 1 = 2)*

(n) Mwalimu alitembea kijeshi.
Juma anacheza kitoto.
} Mwalimu akadirie

*(1 x 1)*

(o)(i) Kijana - Nomino
(ii) Kijana - Kivumishi

*(2 x 1 = 2)*

(p) Mkulima atakuwa akipalilia mihogo.

*(2 x 1 = 2)*

(q) (i) Kichalichali.
(ii) Kochokocho.

*(2 x 1 = 2)*

(r) (i) Kiunganishi
(ii) nafisi

*($2 \times {}^1/_2 = 1$)*

(s) Ni vigumu kwa wanafunzi wasiothamini walimu wao kupita mtihani.

(*al 2*)

**Sehemu ya D:**

**Isimu jamii.**

Mikakati iliyowekwa ni pamoja na;

(i) Kuundwa kwa tume za elimu nchini Kenya kama vile Tume ya Ominde.
(ii) Ongezeko la wandishi wa vitabu via Kiswahili.
(iii) Kushirikisha wanafunzi pamoja na walimu katika maigizo, nyimbo na ukariri wa mashairi katika tamasha za michezo ya kuigiza na muziki kwa kutumia lugha ya Kiswahili kuwasilisha ujumbe.
(iv) Kuhimiza au kutumia Kiswahili katika shughuli za kidini.
(v) Kukitumia Kiswahili kuwasiliana katika vyombo vya habari. (matangazo)
(vi) Waandilizi au watayarishaji wa mitaala au mafunzo katika taasisi ya elimu kutumia zaidi ya lugha moja.
(vii) Kukua kwa utamaduni - lugha ya Kiswahili kutumika.
(viii) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika tasisi za umma / serikali.
(ix) Kiswahili kuwa somo la lazima shuleni.
(x) Lugha ya Kiswahili kutumika bungeni kuwasiliana.
(xi) Lugha ya Kiswahili kupendekezwa kutumika kufundisha masomo yote shuleni au vyuoni.
(xii) lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli au sherehe mbalimbali za kitaifa.
(viii) Tafsiri ya vitabu vya kiingereza kwa lugha ya Kiswahili.

(*zozote 10 x 1*)